

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA AROBAINI NA TATU

13 JUNI, 2022



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA AROBAINI NA TATU – TAREHE 13 JUNI, 2022

I. DUA:

II. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

377. **MHESHIMIWA CHARLES MUGUTA KAJEJE (MWIBARA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itakamilisha majengo ya Shule na Zahanati ambayo yalijengwa kwa nguvu za Wananchi katika Jimbo la Mwibara.

378. **MHESHIMIWA OLIVER DANIEL SEMUGURUKA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-


Je, ni lini Serikali itajenga Stendi Kuu ya Mabasi Bukoba Mjini.

WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:

379. MHESHIMIWA JUDITH SALVIO KAPINGA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:-

Je, kuna mkakati gani wa kuchapisha Sheria za Tanzania katika nakala ngumu na nakala laini ili kurahisisha upatikanaji wa Sheria hizo.



WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

380. MHESHIMIWA HAJI AMOUR HAJI (PANGAWE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukabiliana na matukio ya uhalifu ukiwemo wizi katika Jimbo la Pangawe.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

381. MHESHIMIWA JAPHET NGAILONGA HASUNGA (VWAWA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu,
Sayansi na Teknolojia:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Chuo
cha VETA katika Makao Makuu ya Mkoa wa
Songwe.

WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

382. MHESHIMIWA JOSEPH MICHAEL MKUNDI (UKEREWE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na
Uvuvi:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwezesha
ujenzi wa kiwanda cha kuchakata Samaki
katika Wilaya ya Ukerewe.

WIZARA YA KILIMO:

**383. MHESHIMIWA KENNETH ERNEST NOLLO
(BAHI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kufanya ukarabati kwenye skimu ya kilimo cha mpunga iliyopo Kata ya Bahi.

**384. MHESHIMIWA ZACHARIA PAULO ISSAAY
(MBULU MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, ni lini Serikali itaanza kujenga Bwawa la Umwagiliaji Bonde la Endayaya Tlawi ambapo usanifu wake ulifanyika Mwaka 2007.

WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

**385. MHESHIMIWA MARTHA FESTO MARIKI
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itawaajiri Vibarua wapatao 20 ambao wamefanya kazi Shirika la Reli Mkoa wa Katavi kwa miaka mitano.

**386. MHESHIMIWA CONCHESTA LEONCE
RWAMLAZA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na

● Uchukuzi:-

Je, kuna juhudi gani za kufanya matengenezo ya kudumu katika eneo la Kyabalamba lililopo kati ya Kata za Rubale na Izimbya - Bukoba.

**DODOMA
13 JUNI, 2022**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**